



**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**



Tarehe 02/11/2021

TANGAZO LA AJIRA YA MUDA

Mkurugezi wa Jiji laDar es salaam anawatangazia Watanzania wote wenye sifa, nafasi za kazi ya Uhandisi .(Civil Engineer)

WAHANDISI (CIVIL ENGINEER) NAFASI 6

SIFA ZA KUAJIRIWA

1. Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi
2. Awe na elimu ya Shahada ya Uhandisi kutoka Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.
3. Awe amesajiliwa na bodi ya Wahandisi.
4. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri michoro.
5. Awe na uwezo wa kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha ya Kiswahili na Kingereza.
6. Awe na uwezo wa kuhimili kufanya kazi kwenye presha kadili inavyowezekana na kufanya kazi kwa zamu.

KAZI/MAJUKUMU

1. Atafanya kazi chini ya uanganizi wa Mhandisi aliyesajiliwa wa (profesional engineer) na bodi ya usajili ya Wahandisi ili kupata uzoefu unaotakiwa;
2. Kufanya ukaguzi wa Barabara,Madaraja na Majengo mbalimbali ;
3. Kuchunguza vyanzo vya ajali barabarani;
4. Kufuatilia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za ujenzi wa Barabara na Majengo;
5. Kutayarisha bajeti ya mwaka ya Ujenzi na matengenezo ya Barabara ,Madaraja na Majengo;
6. Kusimamia na kuratibu kazi za Barabara/Madaraja na Majengo zinazotolewa na Mkandarasi.
7. Kuandaa tarifa za utekelezaji wa miradi kwa robo na mwaka

Mshahara kwa mwezi TGS E

MASHARTI YA JUMLA:

1. Awe na cheti cha uraia/namba ya NIDA.
2. Awe na cheti cha kuzaliwa.
3. Awe na umri kati ya miaka 18-45.
4. Awe amehitimu na kupata cheti cha elimu (**Results Slip**) hazitakubalika.
5. Watumishi waliopunguzwa kazi/kufukuzwa kazi/Kuachishwa kazi kwa sababu ya kughushi vyeti serikalini hawaruhusiwi kuomba.

mwajiri ataridhishwa na utendaji wa mtumishi.

Barua zote ziambatane na nyaraka zifuatazo:

Nakala za vyeti vya mwombaji vilivyothibitishwa ambayo ni:

- Cheti cha , kidato cha nne au zaidi
- Cheti cha Taaluma
- Cheti cha Kuzaliwa.
- Kitambulisho cha Taifa
- Picha ndogo mbili (2) za rangi (colored Passport size) za hivi karibuni.
- Waombaji wenye sifa pungufu au za juu hawaruhusiwi kuomba kwani maombi yao hayatafanyiwa kazi.

Barua ambazo hazikuambatanishwa na nyaraka zilizotajwa hapo juu hazitashughulikiwa.

JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

Barua zote za maombi **ziandikwe kwa mkono** zikiwa na anwani kamili ya mwombaji pamoja na namba ya simu zikitaja nafasi unayoomba zitumwe kwa anuani ifuatayo:

MKURUGENZI WA JIJI

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

S.L.P. 20950

DAR ES SALAAM.

Barua za maombi ziwasilishwe Ofisi ya masjala ya Mkurugenzi iliyopo Mtaa wa Mission karibu na jengo la Bandari.

Mwisho kupokea maombi ni tarehe **09/11/2021** Jumanne saa 9.30 Mchana.

Imetolewa na:


Tabu F. Shaibu *KAIMU /MKURUGENZI WA JIJI LA DAR ES SALAAM*

KAIMU /MKURUGENZI WA JIJI LA DAR ES SALAAM

Nakala: Mbao za matangazo Ofisi za Kata – Jiji la Dar es Salaam